

Kuseta kama ilivyotumika kwenye maandiko maana yake ni kukiharibu kitu, aidha kwa kikiponda, kukikanyaga, au Kukivunja vipande vipande.

Kwamfano kwenye maandiko kama haya tunaweza kuona neno hilo..

Warumi 16:19-20

*[19]Maana utii wenu umewafikilia watu wote; basi nafurahi kwa ajili yenu, lakini nataka ninyi kuwa wenyewe hekima katika mambo mema, na wajinga katika mambo mabaya.*

*[20]Naye Mungu wa amani atamseta Shetani chini ya miguu yenu upesi.*

*Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo na iwe pamoja nanyi. [Amina.]*

Hapa Mungu anaonyesha kwamba pale tunapokuwa mbali na mambo mabaya ndivyo anavyomponda shetani chini ya miguu yetu..

Kuonyesha kuwa njia kuu ya kumshinda shetani sio kumkemea bali ni kujitenga na mambo maovu.

Vifungu vingine ni kama hivi..

Zaburi 110:5

[5]Bwana yu mkono wako wa kuume; Ataseta wafalme, Siku ya  
ghadhabu yake.

Hapa Mungu anaonyesha ukali wa ghadhabu yake juu ya watu  
waovu..hata wale wanaoonekana ni wakuu, hawataikwepa hasira yake  
atawaharibu kwa kuwaponda- ponda.

kwa hitimisho ni kuwa kuseta ni kuharibu kabisa Kabisa ..Na Mungu  
amekusudia kufanya hivyo sio kwetu bali kwa shetani... Ni sisi tu kuishi  
maisha yanayomlingana yeye ikiwa tayari tumeshaokoka...Lakini ikiwa  
ni kinyume na hapo tutaingia katika mkondo huo huo wa shetani, wa  
kuharibiwa *endapo* hatutamwamini Yesu Kristo leo.

Je upo tayari kumpokea Yesu leo? Kama ni ndio basi bofya hapa  
>> **KUONGOZWA SALA YA TOBA**

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge na channel yetu kwa kubofya link hii >>

<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Bwana akubariki.

### **Mafundisho mengine:**

*MWEKE SHETANI MBALI NA WEWE.*

*SI SHETANI BALI NI WEWE. (CHAGUA MEMA)*

*DANIELI: Mlango wa 2*

Share on:

WhatsApp